Nuru ya Kiswahili, Juzuu 1(1), Juni 2022: 138 - 157

# Nafasi ya Vipindi vya Redio katika Kukuza Fasihi Simulizi ya Watoto: Mifano kutoka *Watoto Show*

**Shadidu A. Ndossa**
**Mhadhiri, Chuo Kikuu cha St John's cha Tanzania**

shadidu@gmail.com

**Ikisiri**
Makala hii inajadili mchango wa vipindi vya redio katika kukuza Fasihi Simulizi ya Kiswahili kwa Watoto. Makala hii ni matokeo ya utafiti uliofanyika nchini Tanzania. Utafiti ulikuwa na lengo kuu moja, kuchunguza nafasi ya kipindi cha *Watoto Show* katika kukuza Fasihi Simulizi ya Kiswahili kwa watoto. Ili kufikia lengo hili, mambo yafuatayo yalifanyika: Mosi, kubainisha muundo wa kipindi cha *Watoto Show* na namna kinavyotoa fursa kwa vipera vya Fasihi Simulizi ya Kiswahili. Pili, kubainisha vipera vya Fasihi Simulizi vinavyochomoza katika kipindi teule. Tatu, kujadili umuhimu wa vipera hivyo kwa maendeleo ya Fasihi Simulizi ya Watoto. Utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Data zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchambuzi wa matini, ambapo mtafiti alirekodi na kuchambua vipindi 22 vya watoto ili kubaini mambo mbalimbali yanayohusiana na makala hii. Matokeo yanaonesha kuwa vipindi husika vina mchango muhimu katika kukuza Fasihi Simulizi ya Kiswahili kwa Watoto. Kupitia vipindi husika, watoto hupata fursa ya kujifunza hadithi, nyimbo, misemo, vitendawili, vichekesho, na methali.

**Dhana za Msingi:** Vipindi vya redio, *Watoto Show*, Fasihi Simulizi

## Utangulizi

Watoto ni sehemu muhimu ya jamii yoyote duniani. Takwimu za dunia zinaonesha kuwa watoto ni karibu nusu ya idadi ya watu wote waliopo ulimwenguni. Aidha, kundi hili lina fasihi yake maalum inayotofautiana na kundi la watu wazima (Lyimo, 2014). Tangu kale, watunzi wa kazi za watoto wamekuwa wakitumia vionjo maalum katika kazi zao ili kuifikia

hadhira ya watoto. Bakize (2014) anaona kuwa hata kabla ya maandishi, kazi za watoto zilikuwapo ingawa hazikupewa umuhimu mkubwa. Baadaye, kazi za watoto ziliwekwa katika maandishi. Katika namna zote mbili za uwasilishaji, yaani masimulizi na maandishi, watunzi wamekuwa wakitumia mbinu mbalimbali kwa lengo la kuivuta hadhira.

Redio ni njia mashuhuri inayotumika katika kupasha habari mbalimbali. Asilimia 83 ya Watanzania hupata taarifa mbalimbali kupitia matangazo ya redio (Murthy, 2011). Vipindi hivi huwa na mchanganyiko wa vipindi vya watu wazima na watoto. Nchini Tanzania na dunia kwa jumla, vipindi vya redio vina mchango muhimu katika maendeleo ya Fasihi ya Watoto (Mrikaria, 2007). Kupitia vipindi hivyo, watoto hupata fursa adhimu ya kupima uelewa wao katika tanzu na vipera mbalimbali vya kifasihi (Abdallah, 2018). Pamoja na umuhimu huo wa vipindi vya watoto, bado mchango wake haujatambuliwa ipasavyo kupitia tafiti na maandiko mbalimbali. Hivyo basi, makala hii inalenga kujadili nafasi ya vipindi vya redio katika kukuza Fasihi Simulizi ya Watoto.

**Kiunzi cha Nadharia**

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo, utafiti huu umeongozwa na Nadharia ya Uhalisia. Wellek (1961), kama anavyonukuliwa na Wafula na Njogu (2007), anadai kuwa pamoja na mambo mengine, nadharia hii huchunguza mambo halisi yanayojiri katika jamii na namna yanavyoakisiwa katika kazi za fasihi. Aidha, Flaubert (1850), kama anavyonukuliwa na Wafula na Njogu (2007), anasema kuwa ni jukumu la kazi ya kisanaa kuonesha maisha jinsi yalivyo. Hii ni kusema kuwa fasihi ni zao la jamii na hujitokeza katika maisha na hujihusisha na mambo ya kawaida yaliyopo katika jamii. Pia, fasihi hujitokeza na hunogesha vipengele mbalimbali vya kimaisha na kuwa

sehemu muhimu ya maisha ya jamii. Hali hii inasadifiana na namna Fasihi Simulizi ya Watoto inavyochomoza katika vyombo vya habari hasa redio ambapo hujadili na kutathmini mambo mbalimbali ya kijamii. Hivyo basi, nadharia hii imetumika kuonesha namna vyombo vya habari, hasa redio inavyoweza kuchochea watoto kufahamu vipera vya Fasihi Simulizi ya Watoto.

## Methodolojia

Mwandishi ametumia mbinu ya uchambuzi wa matini. Mtafiti alirekodi vipindi 22 vya *Watoto Show* na kuvichambua kulingana na mahitaji ya utafiti. *Watoto Show* ni kipindi cha watoto kinachorushwa kupitia kituo cha *Radio One Stereo*[1] kila siku ya Jumamosi kuanzia saa 3:00 - 4:00 asubuhi. Watoto wengi wanaoshiriki katika kipindi hiki ni kutoka shule za msingi, wenye umri wa miaka minne hadi kumi na miwili.

## Matokeo ya Utafiti

Katika sehemu hii makala inafafanua muundo wa kipindi na ujitokezaji wa vipera vya fasihi simulizi; vipera vinavyochomoza mara kwa mara; na umuhimu wa kipindi husika kwa maendeleo ya Fasihi Simulizi ya Watoto. Kwa ujumla sehemu zote tatu zinaonesha wazi kuwa kipindi cha *Watoto Show* kimesaidia kukuza fasihi ya watoto kama inavyochambuliwa katika sehemu zinazofuata.

### Muundo wa kipindi na ujitokezaji wa vipera vya Fasihi Simulizi

Muundo wa kipindi cha *Watoto Show* umegawanywa katika sehemu kuu mbili. Sehemu ya kwanza, hujumuisha masuala ya kitaaluma. Katika

[1] Radio One Stereo ni redio inayomilikiwa na kampuni binafsi ya *IPP Media*. Kampuni hii inamiliki vituo mbalimbali vya redio, televisheni na magazeti. Baadhi yake ni *East Africa Radio*, *Capital Radio*, ITV, EA TV, Capital TV, Nipashe, na The Guardian, mtawalia. Radio One Stereo ni redio inayosikika eneo kubwa la Tanzania na nje ya Tanzania.

sehemu hii watoto hushiriki kwa kuuliza na kujibu maswali yanayohusiana na masuala ya masomo ya darasani kama vile Sayansi, Hisabati, Historia na Maarifa ya Jamii. Mfano wa maswali ambayo huulizwa katika sehemu hii ni "Tutajie chanzo kimoja cha nishati". Jibu lake ni "jua/umeme/upepo". Kwa kuwa sehemu hii haihusiani moja kwa moja na mada yetu, data zake hazikutumika katika mjadala wa makala hii.

Sehemu ya pili, hujumuisha masuala ya kifasihi na sanaa kwa jumla. Sehemu hii huegemea katika vipera mbalimbali vya Fasihi Simulizi ya Watoto ya Kiswahili. Watoto hupata fursa ya kutamba vipera mbalimbali vya kifasihi simulizi. Katika sehemu hii, vipera vingi vya kifasihi hujitokeza. Baadhi ya vipera hivyo ni hadithi, vitendawili, methali, vichekesho, na mafumbo. Aidha, sehemu hii ya pili imegawanyika katika vijisehemu viwili. Mosi, hujumuisha mjadala wa watoto waliopo studioni ambapo hutamba vipera mbalimbali na kuuliza maswali. Pili, hujumuisha watoto walio majumbani. Watoto hawa hushiriki kwa kupiga simu au kutuma ujumbe mfupi wa maneno kupitia simu za mkononi. Kupitia njia hizi mbili, watoto wa majumbani hupata fursa ya kutamba kazi zao mbalimbali za kifasihi. Jedwali lifuatalo linaonesha muundo wa kipindi hicho kwa muhtasari.

**Jedwali Na. 1: Muundo wa Kipindi Teule**

| Muda | Wahusika | Maudhui | Malengo |
|---|---|---|---|
| Dakika 10 | Watoto wa studioni | Taaluma | Kuongeza maarifa ya shuleni |
| Dakika 10 | Watoto wa studioni | Hadithi | Kutamba hadithi na kutoa funzo |
| Dakika 5 | Watoto wa studioni | Vitendawili | Kutamba na kupata majibu |
| Dakika 5 | Watoto wa studioni | Methali | Kutamba na kupata majibu |
| Dakika 5 | Watoto wa studioni | Mafumbo | Kufumba na kufumbua |
| Dakika 10 | Watoto wa studioni | Vichekesho | Kutamba na kuelezea funzo |
| Dakika 10 | Watoto wa nyumbani na wa studio (kwa njia ya simu) | Vipera mchanganyiko | Kutamba na kupata majibu kutoka studio |
| Dakika 5 | Mtangazaji | Matangazo ya biashara, muziki na maelekezo mbalimbali | Kuwafahamisha wasikilizaji kuhusu bidhaa mbalimbali na burudani |

**Chanzo: Utafiti (2017)**

Jedwali Na. 1 linadokeza mambo mbalimbali muhimu katika mjadala wa makala hii. Mambo hayo ni pamoja na mgawanyo wa muda kulingana na maudhui, vipera vya kifasihi vinavyojitokeza mara kwa mara sambamba na malengo ya vipera hivyo. Kwa kuanza na mgawanyo wa muda kulingana na maudhui; imeonekana wazi kuwa dakika 45 zimetengwa kwa ajili ya vipera mbalimbali vya fasihi. Muda huu ni sawa na 75% ya muda wote wa kipindi. Kwa kuangalia mgawanyo huu, ni wazi kuwa kipindi husika kinatilia mkazo mkubwa masuala ya fasihi ya watoto kuliko mambo mengine. Kwa

kufanya hivi, kunawapa watoto fursa ya kutamba kazi mbalimbali za kifasihi kwa kadiri ya uwezo wao. Katika dunia ya watoto, yapo mambo mengi ambayo mtangazaji angeweza kuyapa umuhimu. Kitendo cha kutenga muda wa kutosha 75%) ni wazi kuwa waandaaji na wasimamizi wa vipindi wanatambua umuhimu mkubwa wa kazi za fasihi katika kuburudisha na kuelimisha. Brand (2007) anaunga mkono hali hii kwa kudai kuwa vyombo vya habari ni muhimu katika maendeleo ya Fasihi ya Watoto. Pia, Ngugi, Lyimo, na Bakize (2019) wanaona kuwa vyombo vya habari hasa magazeti, televisheni na redio ni wadau muhimu wa Fasihi ya Watoto kwa kuwa hutoa fursa kubwa kwa kundi hili kupitia vipindi maalumu vya watoto kwa lengo la kuelimisha na kutoa burudani.

Utafiti huu ulibaini kuna ushiriki mpana wa watoto wa nyumbani kwa njia ya simu. Ilibainika kuwa watoto wanaoshiriki hupiga simu kutoka mikoa mbalimbali. Walikuwepo watoto waliopiga simu kutoka Dar es Salaam, Kigoma, Dodoma, Mwanza, Geita, Singida, Mwanza, Lindi, Mbeya, na Kilimanjaro. Kwa kutumia msambao huu wa ushiriki ni wazi kuwa *Watoto Show* ni daraja zuri la kurithisha amali za jamii kupitia kazi mbalimbali za fasihi zinazowasilishwa (Mlaga, 2017 na Abdallah, 2018). Watoto wengi hushiriki kwa kupiga simu na kutamba baadhi ya vipera vya fasihi. Aidha, wengi wao hupendelea sana kutoa vitendawili, methali na mafumbo. Sababu kuu ya kupenda vipera hivi, pengine, ni kulingana na ufinyu wa muda na kukwepa gharama za kupiga simu kwa muda mrefu. Ushiriki wa watoto kutoka maeneo mbalimbali ni jambo muhimu kwa maendeleo ya Fasihi ya Watoto kwa kuwa unawapa fursa ya kubuni, kutoa na kusikiliza kazi mbalimbali za fasihi.

Uungaji mkono kutoka kwa wazazi ni mkubwa. Data zinazoonekana katika Jedwali Na.1 zinaonesha kuwa wazazi wanaunga mkono suala la watoto kushiriki katika kazi mbalimbali za kisanaa kupitia vipindi husika. Utafiti umebaini kuwa, mara nyingi, idadi ya watoto wanaoshiriki katika kipindi ni kubwa. Hali hii inadhihirika kwa namna mbili. Mosi, watoto wengi hujitokeza studioni. Aghalabu, watoto hao hutoka maeneno mbalimbali katika Jiji la Dar es Salaam. Baadhi ya maeneo hayo ni mbali kabisa na eneo la studio. Mfano, katika kipindi cha tarehe 6 na 13 Januari 2018, walikuwapo watoto kutoka maeneo ya Kibamba, Kigamboni, Mbagala, Temeke, Kimara, na Mbezi Beach. Ukweli ni kuwa kwa jiografia ya Jiji la Dar es Salaam, maeneo tajwa yapo umbali wa zaidi ya kilomita 10 kutoka eneo la studio (Mikocheni). Ni wazi kuwa, ili waweze kushiriki katika kipindi husika ambacho hufanyika asubuhi, inabidi watoto wawahi studioni mapema na wapewe hawa nauli na wazazi/walezi wao. Vilevile, huhitajika ridhaa ya wazazi/walezi ili watoto waweze kushiriki katika kipindi. Pili, uungaji mkono wa wazazi huonekana kupitia ushiriki wa watoto wa nyumbani wanaoshiriki kwa njia ya simu. Watoto hawa huhitaji msaada wa wazazi/walezi ili waweze kushiriki kwa ukamilifu katika kipindi husika. Kwa mfano, watoto washiriki huhitaji kusaidiwa kutafuta idhaa husika na kupewa ridhaa ya kusikiliza redio bila kubughudhiwa ili waweze kupata maudhui ya kipindi na kujua wakati mwafaka wa wao kushiriki kwa kupiga simu. Pia, huhitaji ridhaa ya wazazi katika matumizi ya simu, iwe ni kupiga simu au kutuma ujumbe mfupi wa maneno. Wakati fulani, huhitaji msaada wa wazazi/walezi katika kuweka sawa kazi zao (hadithi, nyimbo, methali) ili ziweze kueleweka kwa ufasaha. Hivyo basi, ni wazi kuwa ushiriki mzuri wa watoto unasukumwa kwa kiasi kikubwa na mtazamo chanya wa wazazi/walezi kuhusu vipindi hivi. Shima (2012), Lyimo (2014), na Ngugi

na wenzake (2019) wanaona kuwa, mara nyingi, wazazi wanao mtazamo chanya na kazi za kifasihi kwa kuwa wanaamini kuwa zina mchango muhimu katika maendeleo ya mtoto kitabia na kitaaluma.

Pia, jedwali linaonesha wazi kuwa kipera cha hadithi kimepewa umuhimu mkubwa. Kati ya dakika 45 zilizotengwa kwa ajili ya masuala ya fasihi, dakika 10 (sawa na asilimia 22) hutumika kwa ajili ya kipera cha hadithi. Sababu kuu ya mgawanyo huu ni kuwa kipera husika huhitaji muda mrefu ukilinganisha na vipera vingine kama vile vitendawili, mafumbo na methali. Kwa wastani, hadithi moja hutumia dakika mbili hadi tatu. Aidha, ilibainika kuwa kila kipindi kimoja huwa na wastani wa hadithi tatu mpaka nne kulingana na urefu wa simulizi za siku hiyo. Maudhui ambayo hujitokeza mara kwa mara ni pamoja na umuhimu wa elimu, heshima kwa wazazi, utunzaji wa mazingira, maisha ya kijijini na changamoto zake, kufanya kazi kwa bidii, na kuepuka tabia ya uvivu. Aidha, kipera cha hadithi hubeba vipera vingine vya kifasihi kama vile nyimbo, utambaji methali na mafumbo (Mulokozi, 1989). Hivyo, ni wazi kuwa, kupitia kipera cha hadithi, watoto hupata fursa ya kujifunza vipera vingine muhimu vya fasihi.
Vilevile, kipindi huambatana na burudani ya muziki/nyimbo. Kipindi kimekuwa kikitenga wastani wa dakika 3 - 4 kwa ajili ya burudani ya muziki. Muziki hutumika katika sehemu tatu: mwanzoni, katikati na mwishoni mwa kipindi. Muziki/wimbo unaotumika mwanzo na mwisho wa kipindi hutumika kama kitambulisho cha kipindi. Aidha, maudhui ya muziki huendana na kipindi husika. Kwa mfano, mara zote kipindi huanza na kumalizika kwa wimbo maalumu. Sehemu ya wimbo huo ni kama ifuatavyo:

Watoto wasafi moyoni
Ni nyota na macho ya wazazi
Sisi ni maua tuliopandwa
Na Mungu Mwenyezi
Laa lalalalala laaa
Laa lalalalala laaa
Laa lalalalala laaa
**Chanzo: Kipindi cha *Watoto Show***

Muziki/wimbo huu unalandana na maudhui ya kipindi husika kwa kuwa unawataja watoto na baadhi ya tabia zao muhimu. Kama ilivyoelezwa hapo awali, wimbo huo hutumika kabla ya kuanza kwa kipindi na mwishoni mwa kipindi kama kiashiria muhimu cha kipindi. Kwa kuzingatia kuwa maudhui ya wimbo huo yanahimiza maadili mema, kinadharia huu ni ushahidi wa wazi kuwa vipindi vya redio vinavyowalenga watoto vina mchango chanya kwa jamii. Mbali na wimbo huo, watunzi wamekuwa wakitumia nyimbo mbalimbali katikati ya kipindi. Nyimbo hizi hulenga kutoa burudani na kuwaelimisha watoto kuhusu mambo mbalimbali yanayowahusu. Kwa mfano, katika kipindi cha tarehe 30 Desemba 2017, ulitumika wimbo wa kundi la *Adaeze and Super Kids*. Baadhi ya beti za wimbo huu zina maneno yafuatayo:

*I love to go to school, to learn to read and write*
*I love to go to school, I want to be a doctor*
*I love to go to school, to learn to read and write*
*I love to go to school, I want to be a lawyer*

*Education is the key, education is the power*
*Education is the key, education is the secret*
*Education is the key, education is the knowledge*
**Chanzo: Adaeze and Super Kids**

Napenda kwenda shule, kujifunza kusoma na kuandika
Napenda kwenda shule, ili niwe daktari
Napenda kwenda shule, kujifunza kusoma na kuandika
Napenda kwenda shule, ili niwe mwanasheria

Elimu ni ufunguo, elimu ni nguvu
Elimu ni ufunguo, elimu ni siri
Elimu ni ufunguo, elimu ni maarifa
**(Tafsiri ya mtafiti)**

Kupitia wimbo huu, kuna mambo matatu muhimu ya kufafanua: Mosi, maudhui yanayotolewa na wimbo huu yanahimiza jambo zuri kwa watoto, hasa suala la elimu. Pili, kwa kuwa wimbo husika ni wa Kiingereza ni wazi kuwa watoto wanapata fursa ya kujifunza lugha ya kigeni kupitia wimbo husika. Tatu, suala la burudani kupitia muziki, wimbo husika uliambatana na mdundo murua ambao watoto huupenda na kuufuatisha kwa kucheza na kurukaruka.

**Vipera vinavyochomoza mara kwa mara**

Kama ilivyodokezwa hapo juu, kipindi teule kinajumuisha vipera mbalimbali vya Fasihi Simulizi. Aidha, utafiti umebaini kuwa kuna vipera ambavyo mara kwa mara vimekuwa vikichomoza na kupewa umuhimu mkubwa katika kipindi. Vipera hivyo ni pamoja na hadithi, vitendawili, vichekesho na methali.

**Jedwali Na. 2: Vipera Vinavyochomoza Mara kwa Mara, Fani na Maudhui Yake**

| Kipera | Maudhui yanayotawala | Vipengele vya kifani vinavyotawala | Mfano |
|---|---|---|---|
| **Hadithi** | Wema dhidi ya uovu, tabia njema, kuheshimu wazazi, sayansi na teknolojia, utunzaji wa mazingira na maisha ya vijijini na changamoto zake | Muundo rahisi, lugha nyepesi, uchanganyaji ndimi, uchanganyaji wa wahusika (watu, wanyama, wadudu na mazimwi), uchanganyaji tanzu | Hadithi ya Sungura na Fisi waliolima shamba pamoja na kupata mazao mengi. Hata hivyo, sungura anamzidi ujanja mwenzake na kutaka kumdhulumu. |
| **Vitendawili** | Tabia njema na kuheshimu wazazi | Takriri, lugha ya picha, urari wa vina, ufundi wa lugha | Ukiona njege utadhani njigi na ukiona njigi utadhani njege. Huku ngo na kule ngo. |
| **Vichekesho** | Tofauti ya maisha ya mijini na vijijini, tofauti za kitamaduni na sayansi na teknolojia | Lugha ya picha, lugha nyepesi, takriri, tanakali sauti, kuiga sauti/lafudhi uchanganyaji tanzu | Kichekesho cha msichana wa kazi kutoka kijijini aliyepika nazi nzima nzima bila kuikuna |
| **Methali** | Tabia njema, umuhimu wa ushirikiano, kufanya kazi kwa bidii | Takriri, lugha ya picha, urari wa vina | Haba na haba hujaza kibaba. |

**Chanzo: Utafiti (2017)**

Katika Jedwali Na. 2 yapo mambo kadhaa yanayojibainisha kuhusiana na matumizi ya vipera vya fasihi simulizi katika kipindi teule. Aidha, ni wazi kuwa matumizi ya vipera hivi yana malengo mahsusi ya kuwafunza watoto fasihi na utamaduni wao kama inavyojadiliwa hapo chini.

***Hadithi***

Kama ilivyoelezwa hapo mwanzo, kipera hiki hupewa nafasi kubwa ukilinganisha na vipera vingine. Kwa upande wa maudhui, hadithi nyingi zilizosimuliwa katika kipindi zilizungumzia mambo yanayoihusu jamii, hasa kundi la watoto. Mfano, kupenda kufanya kazi kwa bidii, kuwaheshimu wazazi, kupinga tabia za kuwanyanyasa watoto, umuhimu wa watoto kula chakula bora, usalama barabarani kwa watoto na nafasi ya watoto katika utunzaji wa mazingira. Katika namna ya kipekee, zilikuwapo hadithi chache zilizozungumzia masuala ya ugunduzi wa kisayansi na athari yake katika maisha ya watu, hasa watoto. Kwa mfano, hadithi zilizohusisha safari kwa kutumia ndege, masuala ya kilimo cha kisasa, matumizi ya simu, televisheni na kompyuta, nishati ya umeme wa jua na ufugaji wa kisasa wa samaki, kuku, na sungura. Ni wazi kuwa maudhui ya hadithi hizi yaliwalenga watoto kwa kiasi kikubwa na mtazamo wao kuhusu dunia wanamoishi. Hali hii ya kuzungumzia mambo yanayowahusu, ndiyo sababu inayowavutia watoto kupenda simulizi hizi. Shima (2012), Bakize (2014), Abdallah (2018), wanaona kuwa hadithi nzuri za watoto ni zile zinazozungumzia mambo ya watoto kwa kugusia mambo ya kila siku yanayojitokeza katika maisha yao.

Vilevile, yapo mambo muhimu ya kifani yanayodhihirika katika hadithi zinazotumika katika kipindi teule. Kwa mfano, mara nyingi, watoto

wamekuwa wakitumia lugha nyepesi na inayoeleweka. Hii ni lugha inayolingana na umri wao kwa kuangalia kigezo cha msamiati na miundo ya sentensi. Pia, wahusika wengi ambao hutumika katika hadithi ni mchanganyiko wa binadamu, wanyama, mazimwi na viumbe wengine. Bakize (2014) na Mulokozi (2017) wanaona kuwa uchanganyaji wa wahusika ni jambo la asili katika kazi za watoto na athari ya wazi kutoka katika muundo wa Fasihi Simulizi. Kwa mfano, katika kipindi cha tarehe 30 Desemba 2017 hadithi zote nne zilizosimuliwa zilijumuisha wahusika mchanganyiko. Aidha, wahusika wanyama ndio waliochomoza zaidi ambapo mhusika sungura na fisi walijitokeza kuwasilisha tabia za ujanja na ujinga, mtawalia.

***Vitendawili na methali***

Utafiti ulibaini kuwa kipindi teule kilitoa fursa ya kutosha kwa watoto kushiriki katika kutoa vitendawili na methali. Aidha, ilibainika kuwa watoto wengi walioshiriki kwa njia ya simu walipenda zaidi vitendawili na methali ukilinganisha na vipera vingine. Kwa mfano, kulikuwa na urejeaji wa mara kwa mara kwa vitendawili ambavyo vinafahamika sana katika jamii. Kwa mfano, “tega nikutege”, “nyumba yangu haina mlango”, “nyumba yangu ndogo lakini ina wapangaji wengi” na “kuku wangu anatagia mibani.” Vitendawili tajwa vilichomoza zaidi ya mara moja katika vipindi vya tarehe 30 Desemba 2017 na tarehe 13 Januari 2018. Abdallah (2018) anaona kuwa vitendawili vinapendwa na watoto kwa kuwa ni kipera rahisi kutamba na majibu yake huwa ni mafupimafupi. Hii ni kusema kuwa watoto wengi wanaweza kuvikariri kwa urahisi ukilinganisha na utanzu wa hadithi ambao ni mrefu na unahitaji hifadhi ya maarifa na stadi ya utambaji. Aidha, Badru (2011) na Ngonyani (2005) wanaona kuwa utanzu huu ni muhimu sana kwa jamii wakiwemo watoto kwa kuwa hutumika kurithisha tunu na amali

muhimu za jamii. Kuhusu umuhimu wa vitendawili, Ngugi na wenzake (2019:54) wanasema:

> Lengo kuu la vitendawili ni kupima elimu ya watoto au kutaka kujua watoto hawa wanajua nini katika uzoefu wa maisha yao … Hivi ni kusema kwamba, maadili, falsafa, mila na mazingira halisi ya jamii huchangia kwa kiasi kikubwa uundaji wa sanaa ya vitendawili.

Pia, vitendawili na methali hutajirisha lugha ya watoto kwa kuwa huambatana na mbinu muhimu za kisanaa kama vile matumizi ya taswira, takriri na urari wa vina. Kwa mfano, kitendawili "nyumba yangu haina mlango", jibu lake ni yai; hapa pana matumizi ya lugha ya picha mbili; yaani, nyumba ambayo haina mlango na yai. Kuweza kuhusianisha picha zote mbili ni jambo linalohitaji uhifadhi wa maarifa na ufahamu wa dhana zote mbili. Vilevile, kuna kitendawili "ukiona njege utadhani njigi na ukiona njigi utadhani njege", jibu lake maziwa na tui la nazi. Katika kitendwili hiki, ni wazi kuwa kuna matumizi kadhaa ya lugha ya kisanaa. Mosi, kuna matumizi ya urari wa vina, yaani mlio wa sauti unaofanana kwa kiasi fulani. Mfano, maneno njege, na njigi. Pia, kuna kukariri maneno, ambapo maneno fulanifulani hurudiwa kwa makusudi, mfano maneno njege na njigi. Tatu, matumizi ya misamiati isiyo ya kawaida. Maneno njege na njigi, kwa kawaida, hayatumiki sana katika mazungumzo ya watoto na watu wazima.

Hali ya kurudiarudia pia ilijitokeza katika utambaji wa methali mbalimbali. Kwa mfano, katika vipindi vya tarehe 4 na 11 Novemba 2017 kulijitokeza methali isemayo "Haba na haba hujaza kibaba." Methali hii inahimiza tabia ya watu kujipinda na kuchuma mali kwa nguvu zao na kuacha tabia ya kupenda mafanikio ya haraka (Abdallah, 2018). Kwa upande wa mbinu ya

kisanaa, kuna matumizi ya takriri, mchezo wa maneno, lugha ya picha na matumizi ya urari wa vina.

***Vichekesho***

Utafiti umebaini kuwa kipindi teule, kwa wastani, kilitoa fursa kwa watoto kuonesha ujuzi wao katika kuwachekesha wenzao. Kwa jumla, maudhui ya vichekesho yalihusu mambo kama vile ushamba wa watu wa vijijini na ujanja wa watu wa mjini, changamoto za sayansi na teknolojia, masuala ya haki za watoto na vioja vya majumbani, safarini, shuleni, na mahakamani. Aidha, muundo wa vichekesho hivi, kwa kiasi kikubwa, ulifanana sana na hadithi. Hii ni kusema kuwa vilikuwa katika mfumo wa masimulizi. Hata hivyo, tofauti na hadithi, malengo ya vichekesho hivi yalikuwa kuiburudisha hadhira na, kwa kiasi kidogo, kuelimisha. Kwa mfano, kama tulivyokwishaona, katika kipindi cha tarehe 2 Desemba 2017 kilitolewa kichekesho cha msichana wa kazi kutoka kijijini ambaye kutokana na kutojua matumizi ya nazi katika kupikia, aliamua kuitumia nazi nzima nzima bila hata kuikuna. Kichekesho hiki kinaendeleza dhana ya mvutano wa maisha ya mjini na vijijini. Senkoro (2011) anaona kuwa mivutano hii ya watu wa mjini na vijijini haiwezi kuisha na itaendelea daima dumu. Watu wengi wa mjini wanajiona werevu na waliopiga hatua kimaendeleo kuliko watu wa vijijini; hivyo, wanatumia fursa hii kuwakejeli. Pia, Ngugi na wenzake (2019) wanashadidia umuhimu wa vichekesho katika fasihi ya watoto kwa sababu ucheshi huibua taswira akilini mwa msomaji/msikilizaji. Hivyo basi, wanahitimisha kwa kumtaka mwandishi wa fasihi ya watoto kudumisha shauku ya msomaji kwa kumfanya acheke pindi anapoanza kuisoma kazi hiyo. Ni wazi kuwa, ingawa waandishi katika nukuu hii wanazungumzia matumizi ya vichekesho katika Fasihi Andishi, hali hii pia hujitokeza katika Fasihi Simulizi.

Kupitia vichekesho, watoto waliweza kuonesha mambo yanayohusiana na sayansi na teknolojia na namna maendeleo hayo yanavyoibua vituko mbalimbali. Hapa walizungumzia masuala ya wizi wa mitandaoni, matumizi ya simu, televisheni, na kompyuta. Aidha, walisimulia vichekesho vinavyoakisi tabia ya wazazi na uhusiano wao na watoto, ndugu na majirani.

Kwa upande wa matumizi ya lugha, ilibainika kuwa vichekesho hutumia lugha nyepesi na, kwa kiasi fulani, hutumia lugha ya picha ili kujenga taswira inayoeleweka kwa wasikilizaji. Kwa kiasi kidogo sana, wachekeshaji walitumia lugha ya kisanaa kama vile methali, nahau na misemo. Pia, kulikuwa na uchanganyaji ndimi, ambapo wachekeshaji wengi waliweza kutumia lugha zaidi ya moja katika uchekeshaji wao, hasa matumizi ya maneno ya Kiingereza. Hali hii inaeleza kwa urahisi utumiaji lugha ulivyo katika jamii, ambapo pana uchanganyaji mkubwa wa lugha hata pasi na sababu za msingi. Aidha, ilibainika kuwa, mbali na uchanganyaji ndimi, kuna ufundi wa uigaji sauti lafudhi wenye lengo la kuibua maudhui fulanifulani na ucheshi kwa wasikilizaji. Kwa mfano, watoto wengi walipenda kuiga sauti za Wahindi, Wazungu na Wachina. Wapo pia walioiga lafudhi za makabila mbalimbali yanayopatikana nchini Tanzania kama vile Wapemba, Wasukuma, Wahaya na Wachaga.

**Umuhimu wa kipindi teule kwa maendeleo ya Fasihi ya Watoto**

Kwa kuzingatia kuwa kuna changamoto kubwa ya upatikanaji wa kazi (vitabu) za watoto katika jamii yetu, kipindi hiki kimekuwa ni msaada mkubwa kwa watoto wa mijini na vijijini. Utafiti ulibaini kuwa kipindi teule kina umuhimu mkubwa kwa maendeleo ya ustawi wa watoto na Fasihi

Simulizi ya Kiswahili. Kupitia kipindi hiki na vipindi vingine, watoto wengi wamepata jukwaa muhimu la kuwasilisha kazi zao. Aidha, kwa kuzingatia kuwa matangazo haya yanasikika maeneo mbalimbali ya ndani na nje ya nchi, kipindi kimeweza kutoa fursa kubwa kwa watoto kujifunza na kufundishana vipera mbalimbali vya kifasihi popote walipo. Kupitia ushiriki wa makundi mbalimbali, kipindi kinatoa ishara kuwa kuna uungaji mkono mkubwa na msukumo wa kijamii katika masuala ya fasihi na sanaa kwa jumla. Hali hii inathibitishwa na ushiriki mzuri wa wazazi, watoto na jamii kwa jumla katika vipindi mbalimbali. Vilevile, kuwepo kwa matangazo mbalimbali ya biashara ni ishara tosha kuwa kipindi kina wasikilizaji wengi hali inayowavuta wadhamini kutoka sekta mbalimbali, hasa zinazohusika na bidhaa na huduma za watoto. Faida nyingine zinazoonekana moja kwa moja kupitia kipindi hiki ni pamoja na hizi zifuatazo:

Kipindi cha *Watoto Show* kinasaidia kukuza lugha ya watoto kwa kuongeza misamiati, kujiamini na uwezo wa kujieleza. Inafahamika wazi kuwa, ili mtoto aweze kusimulia hadithi fulani, lazima awe na uwezo wa kuzungumza lugha husika. Hivyo, ni jambo linalofurahisha kuwaona watoto wakisimulia hadithi kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Vilevile, kipindi husika sio tu kinakuza lugha, bali kinasaidia kufundisha mambo mtambuka yanayofungamana na Fasihi kama vile utamaduni, uzalendo, mazingira, usalama barabarani, na kujiamini. Stadi hizi ni muhimu sana kwa watoto wa karne ya 21 kwa kuwa zinawafanya wawe watu bora na wanaotegemewa katika jamii na taifa kwa jumla.

Zaidi, kipindi husika kinakuza ubunifu wa kifasihi. Kama ilivyojadiliwa huko juu, watoto wamewekwa katika namna ambayo wanaoneka kuwa ndio fanani, hadhira na wachambuzi wa kazi zao. Kwa kufanya hivi, ni ishara tosha kuwa, kipindi kinalenga kujenga msingi bora wa kupata wanafasihi wazuri hapo baadaye.

**Hitimisho**

*Watoto Show* ni kipindi kizuri sana kwa watoto. Kinatoa fursa kubwa kwa watoto kujumuika pamoja na kukuza ufahamu wao wa Fasihi ya Watoto na Fasihi Simulizi ya Kiswahili kwa jumla. Kwa kupitia simu na mawasiliano mengine, kipindi hiki kinakusanya mawazo na uelewa wa watoto kutoka pembe zote za Tanzania. Kuendelea kuwapo kwa kipindi hiki na kuendelea kutoa fursa kubwa kwa tanzu za Fasihi ni uthibitisho wa wazi kuwa Fasihi ya Watoto inayo nafasi muhimu kwa maendeleo ya watoto na jamii kwa jumla. Ni muhimu kwa wadau wote wa fasihi ya watoto hasa wazazi na walezi, walimu, serikali na wamiliki wa vyombo vya habari kuiga mfano mzuri wa kipindi cha Watoto *Show* kwa lengo la kuchangia maendeleo ya fasihi ya watoto.

**Marejeleo**

Abdallah, S. (2017). Uhusika wa Kitoto katika Vibonzo Jongevu: Mbinu ya Kisanaa ya Kuivuta Hadhira ya Watoto.*Mwanga wa Lugha*, 3, 75 - 84.

Abdallah, S. (2018). Muumano wa Hadithi za Fasihi Simulizi na Vibonzo Jongevu: Mfano kutoka katika Akili and Me na Dora the Explorer. *CHALUFAKITA*, 1, 151 - 162.

Adaeze and Super Kids (21 Februari 2014), *education is key*,) http://youtu.be/kx_4x9p-pFQ. Imepakuliwa 16.1.2018.

Bakize, L.H. (2014), *Utangulizi wa Fasihi ya Watoto*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.

Brand, J.E. (2007). *Television Advertising to Children*. Melbourne: The Australian Communications and Media Authority.

Lyimo, E.B. (2014). Nduni za Fasihi ya Watoto: Mifano Kutoka katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto Nchini Tanzania. *Mulika*, 33, 33 - 45.

Mlaga, W.K. (2017). *Misingi ya Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Karne ya 21*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mrikaria, S.E. (2007). Fasihi Simulizi na Teknolojia. *Swahi1i Forum*, 14, 197 - 206.

Mulokozi, M.M. (1989). Tanzu za Fasihi Simulizi. *Mulika*, 21, 1 - 24.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Murthy, G. (2011). *Tanzania Media Environment*. Dar es Salaam: Intermedia.

Ngonyani, D. (2005). Vitendawili vya Kiswahili: Usambamba wake na Dhima yake katika Jamii. *Swahi1i Forum*, 12, 21- 132.

Ngugi. P.M.Y., Lyimo, E.L na Bakize, L.H. (2019). *Fasihi ya Kiswahili ya Watoto: Maendeleo, Nadharia, Mbinu na Mifano ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: TUKI.

Senkoro, F.E.M.K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTU.

Shima, G. (2012). Nafasi ya Vielelezo katika Fasihi ya Watoto, (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri, haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Dodoma.

Wafula, R.M. na Njogu K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.